**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA 1**
**CHETI CHA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI 2024**
**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi 2**
**Machi 2024**
**KIDATO 3 2024**

**MWONGOZO WA KARATASI YA PILI,**

## *1. Ufahamu*

**Maswali**

a. JANGA LA COVID-19/ KORONA/VIRUSI VYA KORONA (1x1=1)

b. Shughuli za kimataifa zilitatizika kwa njia zisizomithilika (1x2=2)

c. Wahudumu wa afya walikosa nafasi ya matibabu au nafasi ya kulazwa katika hospitali wanazohudumu wenyewe. (1x2=2)

d.

i. Watu wengi kupoteza kazi zao.
ii. Watu wengine kutuma kwa likizo bila malipo.
iii. Wengine kukatwa mishahara kwa asilimia kubwa.
iv. Biashara nyingi kufungwa nyingi zikipata hasara chungu nzima.
**v.** Benki kuathirika kwa wateja kushindwa kulipa mikopo.

(zozote 2x1=2)

e.

i. Kukohoa
ii. Kushindwa kupumua au ugumu wa kupumua
iii. Joto jingi au baridi kali mwilini
iv. Maumivu ya misuli au mwili,
v. Kutapika au kuendesha, kupoteza hisia za kuonja na kunusa

Yoyote 1x1=1

f.

i. Kutovaa barakoa kila wakati unapoenda kwenye watu.
ii. Kutokuosha mikono yako kwa maji yanayotiririka na sabuni au kuitakasa.
iii. Kwenda kwenye mikusanyiko ya watu.
iv. Kutozingatie umbali wa mita moja unapokumbana na watu.

3x1=3

g.


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

i. Serikali ilitangaza kufungwa kwa shule.
ii. Kafyu ya saa moja usiku hadi saa kumi na moja asubuhi iliwekwa hapo awali
iii. Kufungwa kwa uchukuzi wa kimataifa kulitangazwa
iv. Kudhibitiwa kwa uchukuzi nchini kwa kupunguzwa kwa idadi ya watu kwenye uchukuzi wa uma.
v. Mikusanyiko ya watu ilipigwa marufuku
vi. Kanisa kufungwa japo kwa muda.
vii. Idadi ya watu katika arusi na mazishi kupunguzwa mno.
viii. Maeneo ya burudani pia yalifungwa kwa muda

Zozote 2x1=2

h.

i) Kafyu ; Amri ya kutotoka nje nyakati fulani haswa usiku hadi asubuhi kama ile ya usiku hadi asubuhi

ii) Ilizirai ; iliziomba/ilizisihia. (2x1=2)

**2. MUHTASARI (alama 15)**

Ufufpisho wa aya za kwanza nne.

Jibu

(a) Mtoto hudhani ulimwengu umejaa raha

(b) Mtoto hajabainisha mambo

(c) Anavyoendelea kukua anabainikiwa na mengi machungu yaletayo huzuni

(d) Ingawa watoto wote hupendwa nyumbani kwao wakosaji huadhibiwa na kuhuzunika

(e) Wanapozembea kazi shuleni huadhibiwa na huhuzunika

(f) Huzuni basi ni uso wa pili baada ya raha

(g) Kila mtu duniani huzongwa na huzuni

(h) Binadamu huchukua huzuni / na hustahabu raha

(i) Raha humjia binadamu kwa nadra ilhali huzuni humvamia wakati wowote.

(j) Kuna watu wengi ambao hawajawahi kuonja raha maishani.

Zozote 8 x 1 = 8

(b) Hali zinazowatia watoto huzuni (aya ya mwisho)


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

i) Wazazi kuaga dunia / kufariki

ii) wazazi walezi wasiojiweza hivyo huzuni tele

iii) Mtoto kutupwa na mama mzazi

iv) Mtoto kulelewa na mama wa kambo mwovu

v) Kulelewa na baba mlevi

Zozote 5x 1 = 5

Jumla

| | | | |
|---|---|---|---|
| | M | (-a) | = 8 |
| | M | (b-) | = 4 |
| Utiririko | | | = 2 |
| | | | 15 |

Hijahi – makosa 6 x ½ = 3 alama

Sarufi – makosa 6 x ½ = 3 alama

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

(a)

(i) /a/ (mwinuko wa ulimi); irabu ya chini

(ii) /i/ (sehemu ya ulimi);irabu ya mbele

(iii) /l/ (namna hewa inavyozuiliwa);kitambaza

(iv) /r/ (ala ya kutamkia); kimadende

4 x ½= 2

(b) i) Pigo moja la sauti katika neno 1x1=1

ii) Silabi funge; silabi inayoishia konsonanti mfano: m-ti

Silabi wazi; silabi inayoishia irabu mfano : m-ti

(2x1=2)

(c)

i) rai; Naomba unileteekikombe kile/ Tafadhali nietee kikombe kile.

ii) masharti; Ukisoma kwa bidii utapita/ Usiposoma kwa bidii hutapita.

iii) amrishi; Toka hapo!/ Tokeni hapo!

(3x1=3)

(d)

(i) mti ; m- umoja

-ti mzizi

(ii) darasani ; darasa; shina

ni; undani/mahali



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

4 x ½= 2

(e)

Nomino ya kitenzijina + kihusishi + nomino ambatani + kitenzi + kiwakilishi
Kulia kwa batamzinga kuliwatisha wote.

1x2= 2/0

(f) Kitoto hiki hiki/hicho hicho/kile kile kinaitwa darasani
(kadiria) 1x2=2/0

(g) Mwanafunzi/mwanagenzi ameng'olewa jino.
kadiria

2x1=2

(h) M-WA; mtoto-watoto
M-MI;mtume mitume
KI-VI; Kiziwi-viziwi
~~O~~-MA;Nahodha-manahodha
~~O~~-~~O~~; shangazi-shangazi

Zozote 2x1=2

(i) Watahiniwa wasingesoma kwa bidii wasingeenda vyuo vikuu. 1x2=2/0

(j) Sara alimsifu/alimpongeza Asna kwa kudai kuwa Bunju alikuwa karimu.

Alama 2x1=2

(k) **''Sitaki** kazi chafu **hapa** Sagamoyo!'' **Majoka** aalisema. Alama 6 x ½= 3

(m) Andika sentensi ifuatayo upya ukizingatia maagizo.
Mtoto alikunywa uji kwa kikombe .
Anza: Uji ulinywewa na mtoto kwa kikombe. 2x1=2

(n) Mwanafunzi alivuta dawati ili aweze kufuta ubao vizuri 1x2=2/0

(o) Asiyesikia la mkuu huvunjika guu

S → KN+KT
KN → N+S
N → ~~O~~
S → Asiyesikia la mkuu
KT → T+N
T → huvunjika
N → guu

8x ½=4

(p)

i) Musa na Amina walicheza./ Musa alicheza na Amina akafua nguo.


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

ii) Mwizi alikamatwa na polisi

2x1=2

(q)

S-S1[KN(N+RV)+KT(T+N)]+U+ S2[KN(W+V)+KT(T+E)]

Mtoto mtukutu sana anachafua nyumba lakini yule mzuri anacheza uwanjani

1x2=2

(r)

Mwanawe wa pili; tendewa

Baiskeli; tendwa

2x1=2

(s) jora 1x1=1

4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(a) Fafanua namna kaida zifuatazo zinavyoathiri matumizi ya lugha katika jamii yako. (alama 10)

i) umri; Vijana hutumia lugha isiyo sanifu, isiokomaa kitamathali, isiyo na heshima, mitindo mipya ya misimu. Wazee hutumia lugha yenye heshima, tamathali, ushauri. Watoto nao hutumia lugha yenye msamiati finyu kutokana na vitu /vifaa katika mazingira yao.

ii) elimu; Mwenye elimu ya juu hutumia msamiati uliopevuka ikilinganishwa na mwenye elimu duni.

iii) mada; Mada rasmi huhitaji lugha sanifu au rasmi .Mada isiyo rasmi inaweza hata kushirikisha msimbo.

iv) uhusiano; wapenzi hutumia lugha ya kupumbaza, mwajiri hutumia lugha ya ukali kwa mwajiriwa wake naye mwajiriwa anatumia lugha ya upole kwake.

v) Hali ya mzungumzaji; Mlevi-Huzungumza kiholela, lugha isiyo na tasfida.Mgonjwa-Huzungumza kwa upole, huruma.(kadiria)



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes